CSSC 2025 MUONGOZO WA USAHIHISHAJI KIDATO CHA PILI

SEHEMU A

1 ALAMA 15

| i | Ii | iii | iv | v | vi | vi | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| D | C | C | B | D | B | B | C | A | B |

2

| I | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| B | G | A | E | C |

3. Mwanafunzi na aeleze misimu tofauti tofauti kutokana na kipindi husika. ALAMA 10@1

MIAKA YA AZIMIO LA ARUSHA

i. Kabaila
ii. Bwenyenye
iii. Ukupe
iv. Mchumia tumbo
v. Ujamaa
vi. Kujitegemea

NJAA YA MWAKA 1974- 1975

i. Unga wa yanga
ii Kufunga mkanda
iii Kumbakumba

KIPINDI CHA MFUMO WA VYAMA VINGI

i. Ngangari
ii. Wapambe
iii. Wakereketwa
iv. Wafurukutwa

AWAMU YA TANO YA SERIKALI YA TANZANIA

i . Hapa kazi tu
ii . Vyuma vimekaza
iii Kazi iendelee

4 (a) Mwanafunzi aoneshe madoido matano (5) yanayopatikana katika nyimbo. ALAMA 10@1

i. Vigelegele
ii. Mishindo
iii. Ala za muziki
iv. Kupiga makofi
v. Sauti ya mtambaji

(b Mwanafunzi na aoneshe mambo matano yakuzigatia katika utumizi sahihi wa lugha

i. Mada ya mazungumzo
ii. Uhusiano baina ya wahusika
iii. Lengo la mazungumzo
iv. Mandhari
v. Umri

5. (a) Mwanafunzi na aoneshe kwa kuelezea vipashio vitano vya lugha ya kiswahili. ALAMA 10@1

i. Mofimu Ni kipashio kidogo kabisa chenye uamilifu wa kisarufi au kileksika mfano, Mama, kaka a-na-som-a
ii. Neno Ni kipashio kinachoundwa kwa mofimu moja tu, au zaidi. Neno likiiundwa na mofimu zaidi ya moja huwa ni neno changamani lenye mzizi na viambishi.
iii. Kirai Ni kipashio kinachoundwa na neno moja au zaidi
iv. Kishazi Ni kipashio kinachotawaliwa na kitenzi kinacho jitosheleza au kisicho jitosheleza Mfano Baba aliyekuja - Kitenzi kisicho jitosheleza Baba amesafiri – Kitenzi kinajitosheleza
v. Sentensi Ni tungo yenye muundo wa kiima na kiarifu inayotoa taarifa kamili Mfano Baba analima shamba

(b) -Tablida Ni mbinu ya kubadilisha mwendelezo wa neno yaani kubadilisha silabi ya mwisho katika neno ili kusawazisha urari wa vina katika kipande bila kuathiri mizani. Mfano,, Yahuzinisha dunia - mara nyingi huwa yahuzunisha duniya

- Inkisari Ni mbinu ya kupunguza idadi ya silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo Siombe badala ya Usiombe

- Mazda Ni mbinu ya kurefusha maneno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo, Mfano Afya ukijaaliwa huwa Afiya ukijaaliwa

- Ritifaa Ni tamathali ya semi ambayo mtu huzungumza na kitu au mtu ambaye yupo katika fikra tu . Mfano Mma mjamzito anaposema ‘ Ewe mwanangu uliye tumboni kua mapema nakusubili hapa nikunyonyeshe’

- Dhihaka Ni tamathali ya semi yenye lengo ya kushusha hadhi na utu wa mtu fulani Mfano, Juma ni mvulana msafi ndio maana nzi wengi wanamfuata

6. Mwanafunzi aoneshe majibu ya vitendawili na nahau kwa ufasaha. ALAMA 10@1

Vitendawili

i. Mtego
ii. Maji
iii. Nazi na mkwezi
iv. Nyota na mwezi
v. Muhogo

Nahau

i. Kujinyonga
ii. Ulimi wenye maneno makali
iii. Kudanganya
iv . Kigeugeu
v . Kuwa na kiburi

7. Mwanafunzi aoneshe maana ya misingi( maana ya awali kabisa na maana ya ziada) ALAMA 10@2

i. Mnyama anayefugwa na binadamu(  msingi)

ii. Kibao cha kukunia nazi

i. Kitendo cha kuketi( Msingi)
ii. Kipande cha moto

i. Kipande cha jani la mti (Msingi)
ii. Kitendo ch kukatisha uhai wa mtu

i. Kifaa kitumikacho kukatia kitu ( Msingi)

ii. Kitendo cha kuweka kitu katika mpangilio (Msingi)

i. Kitendo cha kusia mbegu ( Msingi)

ii. Kitendo cha kukwea mti

8. Mwanafunzi na aoneshe dhima za vivumishi vya pekee katika lugha ya kiswahili. ALAMA10@2
i. Huonesha ujumla wa vitu mfano **ote** katika Maji yote, Jiji lote
ii. Huonesha kitu bila kubagua mfano **o-te** katika Mtu yeyote, Jiji lolote
iii. Hutumika kuonesha umiliki wa kitu mfano **enye** katika Baba mwenye nyumba,
iv. Hutumika kusisitiza nomino fulani mfano **enyewe** katika Mwanafunzi mwenyewe, Mhali penyewe
v. Hutumika kuonesha tofauti mfano **ingine** katika Tunda lingine, Kituo kingine

9. Mwanafunzi na aoneshe miundo tofauti tofauti itokanayo na njia Muambatano kutokana na vigezo alivyopewa. ALAMA 10@1

a. Kitenzi na nomino
- Zima + moto    Zimamoto
- Chemsha +bono    Chemshabongo
- Changa +moto    Changamoto

b. Nomino na nomino
- Mwana+mke    Mwanamke
- Mwana+jeshi    Mwanajeshi
- Panga+boi    Pangaboi
- Mwana+hawa    Mwanahawa

c. Nomino na kivumishi
- Mtu+ mwema    Mtumwema
- Mwenda+wazimu    Mwendawazimu
- Mwana+hewa    Mwanahewa

10. Mwanafunzi na aoneshe sifa mahususi za wahusika wa hadithi za ngano ALAMA 15
i. Huwa na vielelezo vya tabia na mienendo fulani vinavyoendana na tabia za binadamu.
ii. Maranyingi wahusika hawa hawana majina halisi isipokuwa mtu mmoja tu. Mfano Bi kizee Mfalme nk
iii. Mhusika mkuu hupewa jina maalumu au hapewi jina maalumu
iv. Wahusika wake huwa ni wachache sana na hutajwa kwa makundi
v. Wahusika huweza kuwa viumbe hai au wasiwe viumbe hai

vi. Wahusika maranyingi huwa hawapambanuliwi kwa undani zaidi